TANGAZO LA SERIKALI NA. 307 la Tarehe 26/4/2024

SHERIA YA KODI YA MAPATO,

(SURA YA332)

AMRI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA MAPATO KATIKA MRADI WA UJENZI WA BARABARA KUU YA SHELUI - NZEGA NA SONGWE - TUNDUMA KWA KAMPUNI YA M/S NORCONSULT INTERNATIONAL AS, YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Mapato katika Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu ya Shelui - Nzega na Songwe - Tunduma kwa Kampuni ya M/S Norconsult International As, ya Mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 28 Disemba, 2023.

Msamaha

2. Kodi ya mapato inayotokana na kampuni ya M/S Norconsult International As, katika utekelezaji wa mkataba kati ya TANROADS na M/S Norconsult International As kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa barabara kuu ya Shelui - Nzega na Songwe – Tunduma kiasi cha Shilingi za Tanzania 304,786,781.85 kwa Kampuni ya M/S Norconsult International As, imesamehewa.

Ukomo

3. Amri hii itafika ukomo wake baada ya M/S Norconsult International As kuondolewa wajibu wa kulipa Shilingi za Tanzania 304,786,781.85 utokanao na mkataba ulioingiwa chini ya aya ya 2.

Dodoma,
8 Aprili, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
Waziri wa Fedha